**“Everyone’s Different –Respect for Minorities”**

**Episode 01: Zambia’s Pale-Skinned Star**

Author: Adrian Kriesch (HA Afrika) – 4945

Editor: Katrin Ogunsade

Clips: John Chiti (LbE Prod.)

## Characters

| | | | |
|---|---|---|---|
| ***Narrator*** | Mwanamume | Umri wa miaka 30 | english |
| ***John Chiti*** | Mwanamume | Umri wa miaka 27 | english |
| ***Herbert Kirchesch*** | Mwanamume | Umri wa kiasi miaka 50 | german |
| ***Jonathan Muswi*** | Mwanamume | Umri wa miaka 34 | nyanja |
| ***Lista Motokwa*** | Mwanamke | Umri wa kiasi miaka 30 | english |

## Intro

Hamjambo na karibuni katika sehemu ya kwanza ya kipindi chetu kipya cha Noa Bongo Jenga Maisha Yako kiitwacho "**Kila mtu ni tofauti-Kuzingatia maslahi ya jamii za walio wachache**". Katika kipindi hiki chote tutashughulikia makundi mbali mbali na jamii za walio wachache barani Afrika. Wao ni wanadamu kama mimi na wewe, ingawa baadhi yao huenda wakaonekana kuwa tofauti, wana mitizamo tofauti na watu wengineo katika jamii, au wana mawazo tofauti kuhusu maisha, hali inayosababisha wabaguliwe. Hata hivyo, wanaendelea kupigania haki zao. Leo, tutazungumzia uzeruzeru. Hali hii inatokana na hitilafu kwenye ngozi ya mwanadamu ambapo ngozi hiyo hupauka. Mazeruzeru huonekana kuwa na sifa za kipekee hasa barani Afrika. Huwa wanadhulumiwa, na hata kuuwawa, kwa sababu ya imani potofu. Tutakutana na kijana ambaye alibaguliwa utotoni mwake kwa kuwa alionekana tofauti na watu wengine. Lakini sasa hivi ni mtu mashuhuri - ni mtu maarufu nchini mwake.

**1. SFX: John's Song from CD**

**2. O-Ton John Chiti (eng) O1**

*"Jina langu ni John Chiti. Mimi ni zeruzeru, ninaishi Lusaka, nchini Zambia. Mimi ni mwanamuziki na muasisi na Mkurugenzi wa Wakfu wa Mazeruzeru nchini Zambia."*

**3. SFX: John singing a song in the studio**

**4. Narration**

John Chiti anapenda muziki. Sifa hii inadhihirika wazi pindi unapomuona amesimama na kufumba macho mbele ya kipaza sauti kwenye studio yake ndogo. Kibao chake kipya kinahusu mapenzi- **Nyimbo za mapenzi zinachangamkiwa sana nchini Zambia**. Wimbo wa mapenzi ndio uliomfanya kujulikana zaidi mwaka 2008. Wakati huo, John alikuwa ndio amehamia mjini kutoka vijijini. Mara tu alipowasili mjini, mtayarishaji fulani wa muziki alitambua kipaji chake cha uimbaji, na wimbo wake wa kwanza ukawa maarufu papo hapo. Kwa mara ya kwanza maishani mwake, ulemavu wa ngozi wa John ukamfaa vya kumfaa.

**5. O-Ton John Chiti (eng)**

*"Baadhi ya watu walihudhuria onyesho langu, na walikuja moja kwa moja mpaka pale nilpokuwa nikiimbia nyimbo. Walisema; '**Kweli ndiye anayeimba**!' Walidhani nilikuwa nikiigiza sauti. Ninawapa changamoto! Wao hunishuhudia na huu uzeruzeru wangu na husema: **Mashaallah**!"*

**6. Narration**

John alipokuwa mtoto hakupata mtu wa kumsifu na kumhimiza. Baba yake aliitelekeza familia yake punde baada ya John kuzaliwa. Alitatizika sana kwamba mwanawe hakuwa mweusi. Alidhani kwamba mama yake John alikuwa amemwendea kinyume hata akapata mtoto mweupe. Hakujua kwamba mazeruzeru pia huzaliwa na wazazi ambao si mazeruzeru. Wazazi wanaweza kuwa na ngozi ya kawaida, lakini si ajabu damu zao ziwe na chembechembe za nasaba zinazosababisha mtoto mmoja kuwa zeruzeru. Daktari Mjerumani, Herbert Kirchesch anaeleza:

**7. O-Ton Kirchesch (deu)**

*"Hali hii hutokea pale mama anapopata ujauzito. Hakuna utaratibu maalum wa mtoto kupokea chembechembe za nasaba kutoka kwa wazazi wake. Ni jambo la bahati nasibu. Ndiyo sababu kila mtu huwa*

*tofauti na mwenzake. Mazeruzeru huwa na hitilafu kwenye ngozi yao. Hitilafu hiyo haimo kwenye ngozi tu bali pia kwenye nywele na macho."*

**8. Narration**

Mazeruzeru hukabiliwa na matatizo mawili makuu ya kiafya. Kutokana na hitilafu hiyo ya kimaumbile, ngozi zao zimepauka na ni rahisi kuharibiwa na jua. Mazeruzeru wengi barani Afrika hufa kutokana na saratani ya ngozi, kwa kuwa hawapati matibabu mwafaka na pia mafuta yanayokinga ngozi zao zisiunguzwe na jua.  Aidha, mazeruzeru wengi wana matatizo ya macho wala hawana uwezo wa kuona mbali. Huwa wanatatizika kutazama mahali pamoja. Ni muhimu sana kuwaweka mazeruzeru karibu na ubao wa kuandikia wanapokuwa shuleni.

Si matatizo ya kiafya tu yanayowakabili mazeruzeru. Katika mataifa mengi ya Afrika mazeruzeru hukabiliwa na uonevu ama ubaguzi. Kuna imani kadha wa kadha za kishirikina kuhusiana na mazeruzeru - tangu imani kwamba mazeruzeru hawafi hata dhana kwamba nyele za mazeruzeru zinaweza kutibu maradhi. John Chiti anashangazwa sana na visa hivyo. Imani zote hizo ni uvumi usiokuwa na msingi hata kidogo. John, hasa akizingatia maisha yake ya utotoni, anasema kwamba watoto mazeruzeru ndio wanaobaguliwa sana.

**9. O-Ton John Chiti (eng) O4**

*"Sikujichukulia kuwa mtu wa kawaida. Nilijihisi tofauti. Na pindi nilipoanza kuhisi hivyo nilianza kujihoji binafsi. Kulikoni? Kwa nini mimi ni tofauti na watu wengine? Mbona watu wananicheka? Mbona watu wateme mate wanaponiona? Maswali yote haya yanakutatiza. Unaanza kuwa na fikra: Mimi si mtu wa kawaida, sipendwi, mimi sina uzuri wowote. Ninajichukia. Hata kama nilikuwa na uwezo wa kutekeleza jambo fulani, nilivunjika moyo na kusema**: Mimi ni zeruzeru, hili jambo siliwezi**."*

**10. Narration**

John hakuvunjika moyo ingawa laikabiliwa na changamoto zote hizo. Alijikakamua ipasavyo. Katika mwaka wa 2008 alianzisha Wakfu wa Mazeruzeru nchini Zambia. Wakfu huo unajitahidi kuimarisha hali za maisha ya mazeruzeru nchini humo. Wakfu huo una wanachama kiasi ya mia tano. Wengi wao huishi katika mji mkuu, japo John anapanga kufungua ofisi zaidi kwenye miji mingine ili apate kuwahamasisha wakazi katika maeneo hayo pia.

Wanachama hukutana mara kwa mara na kuzungumzia hali ya mazeruzeru. Mazungumzo yao yanalenga kukabiliana na hali ya ubaguzi wa mazeruzeru. Suala hili ni muhimu kushughulikiwa hasa ikizingatiwa taarifa za kila kutwa kuhus mauwaji ya mazeruzeru. Nchini Tanzania, mazeruzeru zaidi ya sitini waliuwawa kati ya mwaka 2007na 2011.

Lengo la wauwaji lilikuwa kuwauzia wachawi viungo vya mazeruzeru.

Uhalifu sampuli hiyo pia umeshuhudiwa nchini Zambia.

**11. SFX Jonathan's house in Kanyama**

**12. Narration**

Tunasafiri hadi Kanyama, eneo la watu masikini katika jiji la Lusaka, ili kukutana na Jonathan Muswi. Bwana huyo mwenye umri wa miaka thelathini na minne (34) ameketi mbele ya nyumba yake, ambapo yeye

na familia yake walikuwa wakiishi hadi mwaka 2011 - mwaka ambao bintiye Prudence aliuwawa akiwa na umri wa miaka mitano.

**13. O-Ton Jonathan Muswi (Nyanja)**

*“Prudence alikuwa akicheza pamoja na marafiki zake. Mama yake alikuwa ameondoka kwenda sokoni. Prudence alikuwa mtoto mpole. Alikuwa akijificha pindi anapoanza ugomvi na wenzake. Mama yake aliporudi, hakumpata. Baadaye, kwenye saa moja hivi, alipatikana maiti kwenye gunia karibu na shule”*

**14. Narration**

Polisi hawakujua dhamira ya kitendo hicho wala hakumkamata mshukiwa yeyote. Hata hivyo, Jonathan Muswi anaamini kwamba binti yake aliuwawa kwa sababu tu ni zeruzeru. Anadhani kwamba mtu aliyemuuwa binti yake alitaka kuuza mwili wake, lakini akalazimika kukimbia bila kuafikia lengo lake. Jonathan anamkumbatia mwanawe mdogo wa kiume. Anasema siku hiyo alipata pigo ambalo hajawahi kupata maishani mwake. Anamkumbuka Prudence kila mara; anajilaumu kwa yaliyotendeka. Kwa sababu na yeye pia hakuhisi vyema pale Prudence alipozaliwa. Alikuwa ndiye zeruzeru pekee katika familia nzima. Jambo hilo lilimtatiza Jonathana si haba! Yeye na mkewe na watoto wao wengine wanne wote ni weusi. Punde baadaye alikwenda kwa ushauri

kwenye Wakfu wa Mazeruzeru ambapo alipewa mafuta ya kulinda ngozi ya Prudence. Alitambua kuwa Prudence hakuwa tofauti na watoto wengineo.

**15. O-Ton Jonathan Muswi (Nyanja)** O5

*"Mazeruzeru ni watu wema. Binti yangu aliuwwaa na umri wa miaka mitano tu lakini niliziona dalili kwamba alikuwa mwema. Nahisi vibaya sana ninaposikia uongo wote unaosemwa kuhusu mazeruzeru. Jinsi watu wanavyofanya biashara ya viungo vyao. Kila ninaposikia hayo, ninakosa raha kabisa."*

**16. SFX: Silence**

**17. SFX: Fade-in Studio Atmo**

**18. Narration**

Ni siku ya Jumapili saa moja na dakika tano jioni kwenye studio ya kituo cha televisheni. John Chiti amechelewa kwa mara nyingine tena. Kipindi chenyewe kimeshaendelea kwa muda wa nusu saa wakati ambapo John anapoingia. Anawasiliana kwa haraka haraka na mtayarishaji na mahojiano yanaanza mara moja.

**19. SFX: Atmo John on stage**

**20. Narration**

Wanazungumzia muziki wa Injili. John amefanikiwa kwa kiasi kikubwa kuandaa muziki wa Injili. Anazungumzia nyimbo zake mpya, muziki wa Injili na pia Mungu. John anajulikana kwa sababu ya muziki wala si sana kumsikia akizungumzia uzeruzeru wake. Kipaji chake hicho cha muziki hakina cha rangi ya ngozi ya mtu. Yeyote anaweza kuwa mwanamuziki.

**KW Anfang**

Baada ya mahojiano, mmoja wa watayarishaji, Lista Motokwa, anatuelezea jinsi ambayo John amebadilisha mitazamo ya raia wa Zambia.

**21. O-Ton Lista Motokwa (eng)**

*"Mtazamo wangu na watu wengineo umebadilika kwa kiasi kikubwa kutokana na watu kama John ambao wamejitokeza na kuzungumzia hali zao waziwazi. Siwabagui mazeruzeru. Hapa mambo huanzia pale unapoendelea kukua. Barani Afrika kuna imani za ajabu kwa mfano watu hudai kwamba mazeruzeru hawafi na kadhalika. Nadhani mitazamo hiyo*

*inabadilika kila kukicha. Mustakabali wa mazeruzeru ni mwema hasa tukizingatia miradi mingi na shughuli nyingi zilizopo za uhamasishaji."*

**22. Narration**

John anasimama karibu na Lista na anakubali kwa kichwa. Anawaomba watu wengine kuwa wavumilivu.

**23. O-Ton John Chiti (eng)**

*"Mazeruzeru ni watu wa kawaida na wanapaswa kutendewa kama watu wengineo. Hakuna mtu hata mmoja anayeweza kusimama kidete na kusema: 'Mimi nimehakikisha kwamba mazeruzeru hawafi.' Mara nyingine mimi huwapa marafiki nywele zangu na kuwaambia: ' Chukueni nywele zangu hizi, mfanye mnavyotaka, tuone ikiwa kweli mtatajirika. Hakuna hata mmoja aliyenijia kuniambia kwamba ametajirika!"*

**KW ENDE**

**24. SFX: Song in the studio** (wimbo unaweza kupigwa chini kwa chini)

**25. Narration**

Mwishoni mwa kipindi, John anaingia jukwaani na kushika kipaza sauti. Wimbo wake mpya wa Injili unaitwa 'Better'. Sasa hivi nchini Zambia hakuna mtazamaji anayesema "Tazameni, huyo zeruzeru!" Watu husema, "Mashaallah – sauti nzuri kama nini!"

**OUTRO**

Na huo ndio mwisho wa kisa chetu cha leo kuhusu uzeruzeru.

Mwandishi wa kisa hiki ni Adrian Kriesch. Ikiwa unataka kusikiliza makala zetu kuhusu kuzingatia maslahi jamii za watu walio wachache, tazama tovuti yetu: dw.de/lbe. Kwaheri, ila usikose kututegea sikio kwenye sehemu itakayofuata!